
# HALMASHAURI YA MANISPAA YA UBUNGO

www.ubungomc.go.tz/Kitengo cha Mawasiliano Serikalini/Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo

# TOLEO MAALUMU MIRADI YA BOOST




HALIUZWI



# BOOST YAINEEMESHA UBUNGO

Na Martha Julius Nicholaus

Serikali inaendelea kutekeleza kwa vitendo Sera ya elimu bila malipo ambayo inazaidi ya miaka nane tangu kuanzishwa kwake lengo ikiwa ni kuhakikisha kila mtoto wa Kitanzania mwenye umri wa kwenda Shule ameanza elimu ya awali.

Katika kutekeleza azma hiyo Manispaa ya Ubungo imeendelea kuboresha miundombinu mbalimbali ya elimu ya awali na Msingi kwa lengo la kuhakikisha mazingira ya ujifunzaji na ufundishaji yanakuwa bora na rafiki kwa wanafunzi na walimu.

Mbali na Manispaa ya Ubungo kuboresha miundombinu mbalimbali ya elimu kwa kutumia fedha za mapato yake ya ndani, pia Manispaa hiyo inajivunia kuwa ni miongoni mwa Halmashauri za Manispaa Nchini ambazo zimepata fedha za BOOST kutoka Serikali kuu kwa ajili ya uborshaji wa miundombinu mbalimbali ya elimu ya awali na Msingi.

'BOOST Primary Student Learning Program' ni Programu yenye malengo ya kuboresha upatikanaji fursa sawa katika ujifunzaji bora wa Elimu ya Awali na Msingi Tanzania Bara. BOOST ni sehemu ya Mpango wa Lipa Kulingana na Matokeo katika Elimu awamu ya pili (EPforR II) na inachangia utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Sekta ya Elimu wa miaka mitano 2021/22 hadi 2025/26.

Manispaa ya Ubungo ilipokea kiasi cha shilingi Bilioni 1.5 kwa ajili ya uboreshaji wa miundombinu ya elimu ikiwemo ujenzi wa Shule mbili mpya za Awali na Msingi Goba Mpakani na Msakuzi Kusini zilizojengwa kwa gharama ya Shilingi 475,300,000 kwa kila Shule

Inaendelea ukurasa wa 02 ....



*Inatoka Ukurasa wa 01*

zikiwa na mikondo miwili yenye madarasa 2 ya awali ya mfano, matundu 6 ya vyoo vya wanafunzi wa elimu ya awali pamoja na bembea za wanafunzi hao, Madarasa 14 ya wanafunzi wa elimu ya Msingi yakiwa na madawati, matundu 16 ya vyoo vya wanafunzi hao, Jengo 1 la utawala na kichomea taka 1.

Pamoja na Ujenzi wa Shule mpya pia Manispaa hiyo ilifanikiwa kujenga madarasa yakiwa na madawati katika Shule mbalimbali za Msingi ikiwemo Shule ya Msingi Milenia ya tatu ujenzi wa madarasa 4 na matundu 4 ya vyoo kwa gharama ya Shilingi 95,200,000, Shule ya Msingi Makoka ujenzi wa madarasa 5 na matundu 6 ya vyoo kwa gharama ya Shilingi 120,800,000, Shule Msingi Mbezi ujenzi wa madarasa 4 na matundu ya vyoo 4 kwa gharama Shilingi 95,200,000, Shule ya Msingi Msumi ujenzi wa madarasa 4 na matundu 4 ya vyoo kwa gharama ya 95,200,000, Shule ya Msingi Matosa ujenzi wa madarasa ya awali ya mfano 2 na matundu 6 ya vyoo, na Shule ya Msingi Makabe ujenzi wa madarasa 4 kwa gharama ya Shilingi 88,000,000.

Na hivyo Mradi wa Boost umeiwezesha Manispaa hiyo kujenga jumla ya vyumba vya - madarasa 49 ya wanafunzi wa elimu ya awali na Msingi yakiwa na madawati na matundu 50 ya vyoo, vyumba 6 vya madarasa ya wanafunzi wa elimu ya awali, matundu 18 ya vyoo pamoja na bembea za wanafunzi hao, majengo mawili ya utawala na vichomea taka viwili.

Manispaa ya Ubungo inajumla ya Shule za Msingi 207 kati ya hizo Shule za Msingi za Umma ni 69 na Shule za msingi binafsi ni 138 shukrani za dhati zimuendee Rais wa awamu ya sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan.









**Pichani ni Viongozi mbalimbali wa Manispaa ya Ubungo akiwemo Mhe. Hashimu Komba Mkuu wa Wilaya hiyo aliyevaa shati la kaki na kofia ya blue, Mhe. Juma Japhary Nyaigesha Mstahiki Meya wa Manispaa hiyo aliyevaa shati la kitenge na Ndg. Elias Runeye Ntiruhungwa Mkurugenzi wa Manispaa hiyo wakitoa maelekezo mbalimbali kwa wasimamizi na wakandarasi wa miradi mbalimbali inayotekelezwa na Manispaa hiyo.**



# UBUNGO YAJENGA SHULE 3 MPYA ZA MSINGI 2023/2024


Na Martha Julius Nicholaus

Manispaa ya Ubungo inajivunia kufanikiwa kujenga Shule 3 Mpya za Msingi ndani ya mwaka wa fedha 2023/2024 ambazo kwa kiasi kikubwa zimesaidia kuwaondolea adha wanafunzi ya kutembea umbali mrefu kufika Shule, kusongamana darasani na hivyo kuwasaidia kuepukana na vishawishi vya njiani, lakini pia zimewezesha uwepo wa miundombinu bora ya kujifunzia na kufundishia.

Miongoni mwa Shule hizo ni Shule ya Awali na Msingi ya Goba Mpakani na Msakuzi Kusini zilizojengwa kwa gharama ya Shilingi 950,600,000 ambazo ni fedha kutoka Serikali kuu za mradi wa Boost huku kila Shule ikigharimu Shilingi 475,300,000 ikiwa na mikondo miwili yenye madarasa 2 ya wanafunzi wa elimu ya awali ya mfano, matundu 6 vyoo vya wanafunzi wa awali pamoja na bembea za wanafunzi hao, Madarasa 14 ya wanafunzi wa elimu Msingi yakiwa na madawati, matundu 16 vyoo vya wanafunzi hao, Jengo 1 la utawala na kichomea taka 1.


Sambamba na Shule hizo Manispaa hiyo imejenga Shule Mpya ya Awali na Msingi ya Kibamba 'B' iliyojengwa kwa gharama ya shilingi 400,000,000 ambazo ni fedha kutoka Serikali kuu ikiwa ni mkondo mmoja yenye jumla ya madarasa 2 ya mfano ya wanafunzi wa elimu ya awali yakiwa na madawati, matundu 6 ya vyoo na bembea za watoto, huku kukiwa na madarasa 7 ya wanafunzi wa elimu Msingi yakiwa na madawati, matundu 16 ya vyoo, jengo 1 la utawala na kichomea taka kimoja.

## MUONEKANO WA SHULE MPYA YA MSINGI YA MPAKANI



**Shule ya Awali na Msingi Mpakani iliyojengwa kwa gharama ya Shilingi 475,300,000 fedha kutoka Serikali kuu za Mradi wa Boost kwa ajili ya ujenzi wa Shule Mpya yenye mikondo miwili ikiwa na madarasa 2 ya awali ya mfano, matundu 6 ya vyoo pamoja na bembea za wanafunzi wa awali, Madarasa 14 ya wanafunzi wa elimu ya Msingi yakiwa na madawati, matundu 16 vyoo vya wanafunzi wa hao, Jengo 1 la utawala na kichomea taka kimoja.**

## MUONEKANO WA SHULE MPYA YA MSINGI YA KIBAMBA 'B'



**Shule Mpya ya Awali na Msingi ya Kibamba 'B' iliyojengwa kwa gharama ya shilingi 400,000,000 fedha kutoka Serikali kuu kwa ajili ya ujenzi wa Shule hiyo ya mkondo mmoja yenye jumla ya madarasa 2 ya awali ya mfano, matundu 6 ya vyoo na bembea za wanafunzi wa awali huku kukiwa na madarasa 7 ya wanafunzi wa elimu Msingi yakiwa na madawati, matundu 16 ya vyoo, jengo 1 la utawala na kichomea taka kimoja.**



MOJA YA MUONEKANO WA NDANI WA MADARASA YA SHULE MPYA ZA MSINGI



MUONEKANO WA SHULE MPYA YA MSINGI YA MSAKUZI KUSINI

**Shule ya Awali na Msingi Msakuzi Kusini iliyojengwa kwa gharama ya Shilingi 475,300,000 fedha kutoka Serikali kuu za Mradi wa Boost kwa ajili ya ujenzi wa Shule Mpya yenye mikondo miwili ikiwa na madarasa 2 ya awali ya mfano, matundu 6 ya vyoo pamoja na bembea za wanafunzi wa awali, Madarasa 14 ya wanafunzi wa elimu ya Msingi yakiwa na madawati, matundu 16 vyoo vya wanafunzi wa hao, Jengo 1 la utawala na kichomea taka kimoja.**

## MUONEKANO WA MADARASA YA AWALI YA MFANO



**UPEKEE WA MIRADI YA BOOST NI UWEPO WA UJENZI WA MADARASA YA AWALI YA MFANO YAKIWA NA VYOO PAMOJA NA BEMBEA ZA WANAFUNZI WA ELIMU YA AWALI, HAKIKA MADARASA HAYO YANAONGEZA ARI YA UJIFUNZAJI NA UFUNDISHAJI**





# MUONEKANO WA BAADHI YA MADARASA YA SHULE MPYA ZA MSINGI HAKIKA SERIKALI IMEFANYA NA ITAENDELEA KUFANYA UBUNGO TUMEWEZA



# HALMASHAURI YA MANISPAA YA UBUNGO

## HALIUZWI

## JARIDA MTANDAO LA TOLEO MAALUMU LA MIRADI YA BOOST

# UBUNGO FAHARI YETU

*yetu*

**JARIDA HILI LIMEANDALIWA NA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI HALMASHAURI YA MANISPAA YA UBUNGO**

**MHARIRI: JOINA JIMMY NZALI**

**MUANDAAJI: MARTHA JULIUS NICHOLAUS**

**MPIGA PICHA: MUSTAPHA H MWAKIBETE**

Tufuatilie kupitia mitandao ya kijamii ya; @ ubungomanispaa

Jarida hili linapatikana kwenye tovuti ya Manispaa ya www.ubungomc.go.tz